

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

+255262963309/13/14
Nukushi: +255 262 963 316
Barua pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz



*Mji wa Serikali, Mtumba,
S. L. P. 2908,
40477 DODOMA.*

TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU NOTISI YA KUSUDIO LA KUTWAA ARDHI CHINI YA FUNGU LA 6 LA
SHERIA YA UTWAAJI ARDHI (SURA 118)**

Dodoma 07 Desemba, 2024

Kupitia Gazeti la Serikali Toleo namba 550 la tarehe 29 Novemba 2024 ilitolewa Notisi kwa Umma kuwa ardhi yenyeye ukubwa wa mita za mraba 233,000 zilizopo Manispaa ya Ubungo na Kinondoni kwenye maeneo yaliyopo katika makutano ya barabara ya Bagamoyo na Kunduchi Mbuyuni (mita za mraba 156,000); makutano ya Sam Nujoma na Chuo Kikuu cha Ardhi Mkabala na Mlimani City (mita za mraba 24,000); eneo lililopo Manispaa ya Ubungo Simu 2000 (mita za mraba 35,000); na Boko Basiaya (mita za mraba 18,000) kuwa inakusudiwa kutwaliwa kwa matumizi ya umma. Maeneo hayo yatahusisha ujenzi wa karakana kuu, maegesho ya magari na vituo vya mrishi.

Kufuatia notisi hiyo baadhi ya wananchi wamekuwa wakitaka kupata maelezo ya ziada kuhusu kusudio la utwaaji huu, utaratibu utakaotumika na namna haki za ardhi walizonazo zitakavyolindwa.

Serikali inapenda kufahamisha umma kuwa, utaratibu wa utwaaji ardhi umebainishwa vyema katika Sheria ya Utwaaji Ardhi (Sura 118). Sheria imeweka takwa la kuwahabarisha wananchi wote ambao ardhi zao zinakusudiwa kutwaliwa kwa ajili ya matumizi/manufaa ya umma ili wawe na taarifa kuhusiana na hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa. **Utekelezaji wa sheria hii umekuwa ukifanyika tangu mwaka 1967 ambapo maeneo mbalimbali yamekuwa yaktwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yenyeye manufaa kwa umma.**

Maeneo yanayokusudiwa kutwaliwa yatatumika kwa ajili ya mradi wa kimkakati wa uwekaji miundombinu ya mradi wa Mabasi Yanayoenda Haraka (BRT) awamu ya nne. Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Mabasi Yanayoenda Haraka (DART). Katika kusimamia utekelezaji wa takwa hilo la kisheria, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa taratibu za kuuhabarisha umma zinafanyika na wananchi ambao ardhi zao zitatwaliwa wanalipwa fidia timilifu, ya haki na kwa wakati kwa kuzingatia Sheria ya Utwaaji Ardhi (Sura 118), Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na.7 ya mwaka 2016.

Matarajio ya Serikali ni kuhakikisha kuwa inaimarisha misingi ya uwazi katika taratibu za utwaaji ardhi ili kuwawezesha wananchi kupata taarifa zinazitosheleza hasa kwenye utekelezaji wa miradi yenyeye manufaa mapana ya Taifa. Aidha, Taasisi za umma zinapaswa kuhakikisha zinafuata taratibu zote za kisheria za utwaaji ardhi.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI